**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*20 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA
## SALAMU ZA POLE

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za rambirambi kwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Jaji George Mcheche Masaju, kufuatia kifo cha Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu, Mhe. Julie Manning, kilichotokea leo, Upanga, jijini Dar es Salaam.

Rais Dkt. Samia amesema Taifa limepoteza kiongozi aliyetoa mchango mkubwa katika kuimarisha misingi ya haki, usawa na uadilifu nchini, na kuongeza kuwa Marehemu atakumbukwa kama kinara aliyefungua milango kwa wanawake wengi kushiriki katika taaluma ya sheria na uongozi.

Ameeleza kuwa, Jaji Manning ataenziwa kwa mchango wake katika mhimili wa Mahakama nchini, akiwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Jaji wa Mahakama Kuu katika nchi za Afrika Mashariki.

***"Tutamkumbuka kwa weledi na uadilifu katika utumishi wake. Ameacha urithi wa mfano bora kwa vizazi vijavyo,"*** amesema Rais Dkt. Samia.

Aidha, ametoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, na watumishi wa kada ya sheria nchini, huku akiwaasa Watanzania kumuenzi Marehemu kwa kuendelea kudumisha misingi ya haki, usawa na utawala wa sheria.

Rais Dkt. Samia anaiombea familia ya marehemu moyo wa subira na ustahimilivu katika kipindi hiki cha majonzi, na kuiombea roho marehemu pumziko la milele.

Shaaban Kissu
K.n.y. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu